# "Nani Aliamua?" Sera ya Lugha na Kitokeacho Mahakamani Tanzania

*Antoni Keya**

**Ikisiri**

*Makala hii inatazama ugumu wa lugha ya sheria na jinsi utekelezaji wa sera ya lugha ya mahakama nchini Tanzania unavyoweza kuathiri juhudi za kutenda haki. Makala imetumia dhamira mbili kati ya tatu za nadharia ya Symbolic Interaction, yaani 'umuhimu wa maana kwa tabia ya binadamu', na 'umuhimu wa kuijenga nafsi kutokana na wenzetu watuonavyo'. Data iliyotumika imetoka kwenye kesi mbili za jinai, na matokeo yanaonyesha kwamba sera ya lugha ya mahakama na mapungufu binafsi huchangia kupunguza ufanisi wa maafisa wa mahakama. Mwenendo uliopo unaweza kuathiri vibaya mtazamo wa jamii kwa mahakama.*

**Dhana za msingi:** *lugha ya sheria, stenokalikimu, Symbolic Interaction, sera ya lugha ya mahakama*

## Abstract

*This article examines how the difficulty in legal language and the traps inherent to the legal personnel in effecting the Tanzanian legal language policy is likely to inhibit the dispensation of justice. The article uses two themes of Symbolic Interaction Theory, that is, 'the importance of meanings for human behaviour', and 'the importance of the self-concept' focusing on the assumption that individuals develop self-concepts through interaction with others. Data were drawn from two criminal cases, and results show that both individual linguistic weaknesses of legal personnel and the demands of the legal language policy make justice extremely hard to realize.*

**Keywords:** *legal language; stenokalikimu; Symbolic Interaction; legal language policy*

## Utangulizi

Makala hii inatazama jinsi utekelezaji wa sera ya lugha ya mahakama nchini Tanzania unavyoweza kufanikisha au kukinzana na juhudi za kutenda haki kwa wanaoitafuta haki kupitia mahakama, hasa wanaohojiwa kama washitakiwa au mashahidi. Utekelezaji wa sera hii unatazamwa sambamba na jinsi majaji na mahakimu wanavyotekeleza majukumu yao ya kusimamia mwenendo wa kesi kufuatia matakwa ya Sheria ya Ushahidi. Ili kufanya hivi, makala hii

* Mhadhiri, Idara ya Lugha za Kigeni na Isimu, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, S.L.P. 35040, Dar es Salaam, Tanzania, Barua pepe: amkeya@yahoo.com

inaanza kwa kuutazama ugumu wa lugha ya sheria na sera ya lugha mahakamani, kisha inachambua matini juu ya mazingira ya kimahakama na mahojiano-bomozi yafanyikayo kati ya shahidi na wakili. Kabla ya kuchambua data na kufanya majadiliano, makala hii inaongelea kidogo nadharia, kisha inaangalia kitokeacho mahakamani kwa kuangalia majukumu anayopaswa kuyatekeleza jaji wakati wa shauri. Baada ya hapo kuna hitimisho na uwasilishaji wa marejeo.

## Ugumu wa Lugha ya Sheria na Sera ya Lugha Mahakamani

Kuna vyanzo viwili vya ugumu katika mawasiliano ya kisheria: cha muhimu zaidi katika mada hii ni kwamba "wasio wanasheria hawawezi kuielewa lugha ya sheria" (Gibbons, 2003:165). Waandishi wengi wanakubaliana kwamba lugha itumikayo kisheria ni ngumu kwa wasio katika fani ya sheria. Kwa mfano, Jackson anasema kwamba "mbali na kwamba sheria ya Kiingereza inawasilishwa zaidi kwa lugha ya Kiingereza, wazungumzaji wengi zaidi wa Kiingereza wametengwa na matumizi ya lugha ya kisheria kwa sababu hawawezi kuelewa aina ya lugha itumikavyo" (Jackson 1990:87, kama alivyonukuliwa na Gibbons 2003:162). Mellinkoff yeye anasema kwamba "[Kiingereza cha sheria] kina mbwembwe za maneno mengi, hakieleweki, ni cha kujidai na hakivutii kabisa" (Mellinkoff 1963, kama alivyonukuliwa na Gibbons, 2003:162).

Suala hili la ugumu wa lugha ni muhimu kwa kuwa sheria tunayoifuata Watanzania inasema kwamba kutojua sheria hakuwezi kuchukuliwa kama kisingizio cha kutenda kosa, kwa hiyo sheria isipowasilishwa wazi wazi kwa inaowahusu nachukulia kwamba ni kinyume cha haki.

Gibbons anangalia kazi za kisanaa ambazo zimekosoa sheria, kama vile *Gulliver's Travels* (Jonathan Swift) na sinema mbili za *Animal Crackers* na *A Day at the Races* (Marx Brothers), pamoja na *Bleak House* ya Charles Dickens. Eagleson anasema kwamba mbali na kutoeleweka kwa wasio wanasheria, lugha ya kisheria haieleweki hata miongoni mwa wanasheria wengi. Wengineo wanaoongelea mada hii ni Bentham (1838), Mellinkoff (1963), na Renton (1975) (Gibbons, 2003:163). Matatizo ya ugumu wa lugha ya sheria haiko kwenye lugha ya Kiingereza pekee. Duarte i Montserrat (1993) na Duarte i Montserrat na Martinez (1995) wanaonyesha ugumu wa lugha za Catalani na Kihispania kwenye sheria; Cavagnoli na Wölk (1997) huonyesha matatizo hayo hayo katika Kiitaliano. Gunnarsson (1984)

huonyesha matatizo ya Kiswidi kitumikacho kwenye sheria; huku Okawara akionyesha jinsi Kijapani cha kisheria kilivyo kigumu kwa Wajapani wa kawaida (Gibbons, 2003:164).

Kuielewa na kuizungumza lugha huangukia kwenye masuala ya uelewa wa lugha. Elimu ni mazingira ya msingi ambayo humwezesha mtu kuwa na usahihi wa lahaja ya juu (kama ya kisheria), kwa hiyo wasio na elimu ya kutosha wana nafasi ndogo sana katika mawasiliano haya. Watu wa namna hii hasa ni watoto na wanaoongea lugha isiyo fasaha (yenye mchanganyiko au athari za mahala watokako). Wanaoteseka zaidi ni wale ambao hawajasoma kabisa, ambao hukadiriwa kuwa asilimia 7 katika nchi nyingi, na ndio wengi wao hushtakiwa kwa makosa ya jinai (Hayes, 1993 kama alivyonukuliwa na Gibbons, 2003:201). Kwa kuwa mfumo wa sheria ya mapokeo ya Kiingereza tunaoufuata "unasemwa zaidi…sheria na mikataba huongelewa zaidi mahakamani, hivyo kudhihirisha zaidi ugumu wa lugha ya sheria" (Gibbons, 2003:201).

Sera ya lugha ya mahakama Tanzania, kwa mujibu wa Sheria ya Mahakimu ya Mwaka 1984 13(1–2), ni kwamba Kiswahili kitatumika kusikiliza mashauri na kuandika maamuzi katika Mahakama ya Mwanzo, wakati Kiingereza na Kiswahili vitatumika mahakama za juu, yaani Mahakama ya Wilaya, Mahakama ya Hakimu Mkazi, Mahakama Kuu, na Mahakama ya Rufaa. Katika mahakama hizi za juu majadiliano yanaweza kufanyika katika mojawapo ya lugha hizi mbili, lakini mwenendo wa shauri pamoja na maamuzi lazima viandikwe kwa lugha ya Kiingereza. Nafasi ya Kiswahili kutumika kuweka kumbukumbu za mashauri na maamuzi yake huishia Mahakama ya Mwanzo. Katika mahakama za juu, hata hivyo, majadiliano au mwenendo wa kesi hufanyika katika lugha mojawapo baada tu ya wahusika katika shauri kukubaliana kwamba shauri liendeshwe kwa lugha hiyo. Hata ukalimani unaofanyika mahakamani ni kuelekea kwenye mojawapo ya lugha hizi. Itokeapo kwamba wahusika wanaweza na wanajisikia huru kutumia lugha ya Kiingereza, baadhi ya majaji hupendelea shauri lifanywe kwa Kiingereza ili iwe rahisi kwao kunukuu maneno ya wahusika. Kwa mwonekano uliopo, si rahisi kusikia malalamiko juu ya mtu kulazimishwa kutumia lugha asiyo na uwezo nayo.

**Mahojiano na Mazingira ya Mahakamani**
Tafiti nyingi juu ya mahojiano ya mahakamani (kv. Beach, 1985; Danet, 1980; Dunstan, 1980; Goodman *na wenzake,* 1998; Hale & Gibbons, 1999; Konradi, 1996; Luchjenbroers, 1991; Matoesian, 1993; Penman, 1987; Rigney, 1999; Wahn & Clayton, 1996; na Walker, 1987) zimeonyesha kwamba kutokana na msigishano mkubwa uliopo kwa nyanja tofauti kati ya wahusika (ikiwamo weledi wa matumizi ya rasilimali lugha), hali ya shahidi huwa tete wakati wa mahojiano-bomozi, kwa kuwa si rahisi kwake kutoa ushahidi kwa kiwango kinachostahili. Wengine huutazama ukumbi wa mahakama (jinsi ulivyopangwa na shughuli zinavyofanywa humo) na kusema kwamba unachangia pia kumfanya shahidi asiwe na ujasiri ambao angekuwa nao nje ya maeneo ya mahakama. Maley, kwa mfano, anafananisha hali ya mtu mgeni mahakamani na mtu aliyeingizwa ghafla kwenye dunia ngeni yenye vitu vingi vya kutisha (Maley, 1994:32).

Hirsch (2001), Maley (1994), na Luchjenbroers (1991) wanaamini kwamba jinsi mahojiano yanavyofanywa hupunguza sana uwezo wa shahidi kujieleza kwa uhuru. Marshall *na wenzake* (1971) wanasema kwamba katika mazingira ya mahakama mashahidi kwa kawaida huwa na kiwango fulani cha msongo ambacho hupunguza uwezo wao wa kuwasiliana na hivyo kuathiri ubora wa ushahidi wao (Marshall *na wenzake* 1971:1634). Kutokana na ushindani uliopo kwenye mahojiano-bomozi, wasomi wengi wameibuka na sitiari nyingi za kuyaita mahojiano haya, kama vile: *vita yenye ushindani mkubwa sana wa kiakili* (Kirchheimer, 1969:342; Maley, 1994:32–3), *mashindano ya kusimulia hadithi* (Woodbury, 1984:206) na *mpambano wenye madhara makubwa* (Drew, kama alivyonukuliwa na Freedgood, 2004:4). Kwa kuwa hali ya mahakama ya Tanzania si tofauti na hali iliyoelezwa hapa, ni vema kuzingatia hali hii tutazamapo kinachotokea mahakamani.

**Nadharia Iliyotumika**
Nadharia iliyotumika kuchambua data na kujadili matokeo ni Alama kama Msingi wa Mawasiliano (yaani *Symbolic Interaction Theory*). Nadharia hii "husaidia kuelewa jinsi ambavyo binadamu hushirikiana katika kuumba maana, na jinsi ambavyo maana hizi huathiri tabia" (LaRossa & Reitzes, 1993:136). Ni daraja linaloonyesha utegemezi kati ya mtu mmoja na jamii. Wananadharia hawa (wakiongozwa na Mead) wanaamini kwamba hakuna kitu kilicho na maana zaidi ya ile kinayopewa na binadamu / jamii, na kwa hiyo wanaangalia maana

kama mali ya jamii. Kwa maana nyingine, kama tutakavyoona kwenye stadi hii, maana wanazotengeneza watu zinatokana na kukutana kwao na shughuli za kimahakama huathiri jinsi wanavyoitazama mahakama.

Stadi hii hutumia dhamira mbili kati ya tatu za nadharia hii. Dhamira ya kwanza ni ielezayo *umuhimu wa maana kwa tabia ya binadamu,* nikisisitiza mtazamo kwamba *maana hujengwa kutokana na mawasiliano baina ya watu.* Dhamira ya pili ni *umuhimu wa kuijenga nafsi,* ambayo husema kwamba *binadamu hujijenga nafsi kupitia mawasiliano yao na wengine*, na pia kwamba *kujijenga nafsi ni msingi wa kujenga tabia*. Mead anasema kwamba vyovyote tunavyojitazama nafsi zetu inatokana na mtazamo wenzetu walionao juu yetu. Anaazima wazo la Charles Cooley la *nafsi hutokana na kujitazama kwenye kioo* (yaani *looking-glass self*), akisisitiza kwamba uwezo wetu wa kujiona unategemea na wengine wanavyotuona.

**Data na Majadiliano**

Makala hii inarejea mifano kutoka kwenye kesi mbili: Kesi ya Jinai namba 95 ya 2008, Jamhuri dhidi ya Mwita Sangali; na Kesi ya Jinai namba 26 ya 2006, Jamhuri dhidi ya ACP Zombe na wengine 12, ijulikanayo zaidi kama "Kesi ya Zombe". Kesi hizi zinatumika kuonyesha umuhimu wa mwamuzi kuwa mwangalifu ili kutambua matatizo yatokanayo na matumizi ya lugha, na matatizo yanayoweza kujitokeza endapo jukumu la kuangalia kwamba mahojiano yanafanyika kwa haki halitafanywa kwa ukamilifu. Tuanze kwa kutazama kitokeacho mahakamani na kisha tumtazame jaji kama mkalimani.

**Kitokeacho Mahakamani Tanzania**

Mbali na hali iliyoelezwa hapo juu kuhusu mahojiano na mandhari ya mahakama kutokuwa rafiki kwa shahidi, kipengele hiki kinapitia utekelezaji wa sera ya lugha katika mazingira yaliyobainishwa hapo juu, na kutazama jinsi jaji anavyotekeleza majukumu yake sambamba na sera hii ya lugha. Makala hii inabainisha baadhi ya ugumu unaoukabili mfumo wa haki chini ya sera hii ya lugha.

Sheria ya Ushahidi inamtaka jaji daima asome haiba ya shahidi wakati mahojiano yakiendelea (Evidence Act, 2002). Kinyume na matazamio, hili si jukumu rahisi katika mazingira ambapo shauri huendeshwa kwa Kiswahili, katika mahakama ambazo hakuna mstenografia (mwandishi wa mahakama) na mitambo ya kunasia

sauti. Kwa kuwa mwenendo wa shauri unatakiwa uhifadhiwe katika lugha ya Kiingereza, jaji anakuwa na majukumu mengi zaidi, mbali ya kuwa mwamuzi. Hapa ndipo changamoto huanzia. Kwanza, jaji atapaswa kufanya ukalimani (japo anachofanya hakiendi sambamba na utafsiri [translation] na ukalimani [interpretation]), pamoja na ustenografia. Wakati haya yote yanafanyika, jaji anapaswa pia kuendelea kutekeleza jukumu lake la *kusimamia uendeshaji wa shauri* huku akihakikisha kwamba kanuni zote hufuatwa, akiamua aina ya ushahidi unaostahili kupokelewa, muundo wa uulizaji maswali, na kuhakikisha kwamba hakuna mshiriki anayetenda au kutendewa kinyume na haki (Magenau, 2004:39). Changamoto zinazosababisha jaji au hakimu alazimike kutekeleza majukumu haya yote ndizo zinazozaa jina jipya la jaji au hakimu kama *mstenokalikimu*, yaani mstenografia anayefanya ukalimani na hatimaye kutoa hukumu.

Makala hii inajikita zaidi kwenye majukumu mawili: ukalimani na usimamizi wa mwenendo wa shauri. Inaangalia pia kwa karibu uwezo wa jaji kuyatekeleza majukumu yake yote kwa pamoja. Lakini pia makala hii inajengwa juu ya imani kwamba ili jukumu la usimamizi wa mwenendo wa shauri litendeke vema, jaji anahitaji, mbali na mambo mengine, ajielekeze kwenye kudhibiti matumizi ya lugha ambayo yanaweza kufanya mchakato wa mahojiano uelemee upande mmoja kutokana na umahiri au ukorofi wa mmojawapo wa washiriki katika matumizi ya rasilimali lugha. Jaji hatafanikiwa kufanya hili kiufasaha endapo yeye mwenyewe hatakuwa na uwezo wa kugundua mitego itokanayo na matumizi ya rasilimali lugha. Ni jukumu la jaji kuhakikisha kwamba mtu hashindwi shauri kwa kupungukiwa weledi wa matumizi ya rasilimali lugha (Magenau, 2004:39).

**Jaji kama Mkalimani**

Fani ya ukalimani inahitaji kwamba mkalimani awe na uelewa wa kutosha wa lugha zote mbili zinazohusika. Ni rahisi kiasi kusema kiujumla kwamba majaji wa Tanzania wanaifahamu kiasi kikubwa lugha ya Kiswahili, japo si kwa kiwango cha wanaisimu na walio kwenye nyanja nyinginezo za utaalamu wa lugha. Hii naisema kwa tahadhari kubwa kwa kuwa hakuna uthibitisho kwamba wasemaji wa Kiswahili wote wanakifahamu Kiswahili ipasavyo, kama itakavyothibitishwa na data kwenye makala hii. Nisicho na uhakika nacho hasa, ni kiwango cha majaji cha umahiri katika lugha ya Kiingereza, ambacho kwa mtazamo wa kisera kinaonekana kama

lugha mama ya mahakama zetu. Ili mtu kuwa hakimu, wakili na hata jaji, hakuna hitaji lolote lililowekwa kwamba awe na kiwango fulani cha elimu au ujuzi wa masuala ya ukalimani au utaalam wa lugha kwa ujumla. Hata sasa, si dhahiri endapo mahakama inapanga kuwapa mahakimu na majaji mafunzo ya muda mfupi mara waanzapo kazi ili kuinua kiwango chao cha utaalamu katika masuala ya lugha. Kwa hiyo si vema kujiaminisha tu kwamba ukalimani hufanyika kiusahihi na kila mhusika. Msingi wa hofu hii ni upi?

Nitatoa mfano mmoja. Nilipokuwa nahojiana na jaji mmoja wa Mahakama Kuu ya Tanzania wakati wa utafiti (tofauti na huu), alinipa mfano ufuatao, ambao alisema ulitokana na kisa cha kweli. Hakimu mmoja alimsikia shahidi akidai kwamba kilichomfanya amtambue mshitakiwa ni kwamba siku ya tukio mshitakiwa alikuwa amevaa suruali yenye viraka vingi. Hakimu hakuweza kupata neno la Kiingereza la 'viraka vya nguo' kiurahisi. Ghafla ilimjia kichwani kwamba Katiba ya Tanzania ya mwaka 1977 imekuwa ikisemwa kwamba ina 'viraka' vingi sana, ambapo neno la Kiingereza ambalo huwa linatumika ni 'amendments'. Kwa hiyo hakimu akaandika, "because his trouser[s] had many amendments".

Wakati kwenye Kesi ya Jinai namba 95 ya 2008 hakukuwa na ukalimani legelege kama mfano huo hapo juu, jaji katika kesi hii aliashiria kwamba yeye pia anatambua ugumu na madhara ya *kustenokalikimu* yanayotokana na mkanganyiko wa sera ya lugha mahakamani. Alipotaka kusoma hukumu alitoa angalizo, "Hukumu yenyewe nimeiandika kwa Kiingereza, lakini nitaisoma kwa Kiswahili. Kwa hiyo tusameheane nitakapokosea." Hapa jaji hakutaja tu kwamba ustenokalikimu ni safari ndefu, na kwamba alikuwa amesikiliza kila sehemu ndogo ya shauri kwa Kiswahili kabla hajaihamishia kwenye Kiingereza. Urefu wa safari hii unazua shaka moja. Je, katika safari hii ndefu ya kuhamisha kauli za washiriki kutoka Kiswahili kwenda Kiingereza na hatimaye hoja na maamuzi kufanywa kwa msingi wa kilichonukuliwa kwa Kiingereza, na kisha tena kukihamisha hiki na kukisema kwa Kiswahili hufanyika bila kupunguza, kuongeza au kupindisha maana ya kilichosemwa kwenye mahojiano? Wakati twaweza kusema kwamba kunaweza kusiwe na msigano mkubwa sana kimaana kati ya akisemacho jaji kwa Kiswahili kutoka kwenye Kiingereza chake mwenyewe, si rahisi kusema kwamba hakuna kipoteacho, kuongezeka au kupinda anapofanya ukalimani wakati wa mahojiano. Wakati vilevile inatambulika kwamba si rahisi mara zote kupata asilimia 100 ya

maana iliyokusudiwa, hali yaweza kuwa mbaya zaidi ambapo kiwango cha uelewa wa lugha husika cha mstenokalikimu si cha kuridhisha.

Shaka hiyo inakuzwa na kifuatacho. Wakati shauri likiendelea, uchanganyaji misimbo wa jaji kwenye mojawapo ya kesi ninazozirejea hapa ulibainisha kwamba kiwango cha jaji cha utaalam wa lugha kilikuwa cha kutia shaka japo kidogo. Katika moja ya matukio, kwa mfano, akitaka kujiridhisha kwamba ameielewa vema hoja aliyotoa mmoja wa mawakili, jaji aliuliza kwa Kiingereza, "What did she done?" (akimaanisha "Alifanya nini?") badala ya kusema, "What did she do?" Ni vigumu sana katika mazingira kama haya kumwona mstenokalikimu akihamisha majibu ya shahidi kutoka Kiswahili kwenda Kiingereza kwa usahihi usiotia shaka. Tatizo zaidi ni kwamba endapo mmojawapo wa washiriki hataridhika na maamuzi akakata rufaa, rufaa itafanywa juu ya hukumu aliyoiandika jaji. Endapo hukumu hii ni matokeo ya ukalimani dhaifu inaweza kuwa na mapungufu ambayo yatafanya haki ya mlalamikaji ipotee.

**Jaji kama Msimamizi wa Mahojiano**

Hatua ya pili, huangalia endapo asimamiapo mwenendo wa shauri (ikiwa ni pamoja na kuona kwamba maswali yanaulizwa kiusahihi), jaji huhakikisha kwamba matumizi ya rasilimali lugha hayamweki anayehojiwa kwenye nafasi tete. Kwa mfano, katika Kesi ya Jinai namba 95 ya 2008, mahojiano-bomozi kati ya mshitakiwa na wakili yalikuwa hivi:

| | |
|---|---|
| **WAKILI:** | Wakati marehemu anakumwagia mchanga ulikuwa umelewa? |
| **MSHITAKIWA:** | Marehemu hakunimwagia mchanga. |
| **WAKILI:** | Wakati marehemu anakumwagia mchanga ulikuwa umelewa? |
| **MSHITAKIWA:** | Hunielewi? Nimekwambia hakunimwagia mchanga! |
| **WAKILI** | (akimgeukia jaji): Mheshimiwa, mshitakiwa hataki kujibu swali langu. |
| **JAJI** | (akimwelekea mshitakiwa): Jibu swali! |
| **WAKILI:** | Wakati marehemu anakumwagia mchaga ulikuwa umelewa? |
| **MSHITAKIWA:** | Hapana. |

Katika majibizano hayo hapo juu, mshitakiwa aliubaini mtego aliowekewa na wakili. Swali aliloulizwa lina hoja mbili, na

mshitakiwa hakukubaliana na mojawapo ya hoja hizo. Kwa hiyo ilikuwa hatari kulijibu swali kwa 'ndiyo' au 'hapana' kama alivyotaka wakili. Kwa mshitakiwa kujibu tu 'ndiyo' au 'hapana' ni kukubaliana na hoja ashiria *(presupposition)* kwamba kitendo cha kumwagiwa mchanga kilifanyika. Kwa kuchelewesha jibu lililongojwa na wakili, mshitakiwa alitaka swali lirekebishwe kwanza, akiwa na shaka sahihi kwamba kujibu 'ndiyo' au 'hapana' haikuwa sahihi. Wakili alifanya ionekane mbele ya jaji na wazee wa baraza kwamba yeye alichotaka kujua ilikuwa tu endapo mshitakiwa alikuwa amelewa. Hoja kwamba alirushiwa mchanga na marehemu ilichukuliwa kuwa ni kitu kilicho wazi kisichohitaji mjadala. Hii haikuwa sahihi kwa haki ya mshtakiwa, kwa kuwa katika mahojiano yote hakuna mahala mshitakiwa alipokuwa amedai kwamba alimwagiwa mchanga. Jaji hakustahili kumlazimisha mshitakiwa kujibu swali ambalo halikuwa sahihi.

Yawezekana, hata hivyo, kwamba jaji alipoamuru mshitakiwa kujibu swali hili alikuwa amepotoshwa na mwonekano wa swali. Swali hili lilifanana kijuujuu na maswali-chambo kwa kuwa lenyewe pia lilidai jibu la 'ndiyo' au 'hapana'. Kwa kuwa maswali ya namna hii ndiyo yatumikayo zaidi kwenye mahojiano-bomozi, jaji alidhani linastahili kujibiwa, kama vile 'Je, ulikuwa umelewa?'. Alipotoka. Alistahili kuhakikisha kwamba maswali sahihi ndiyo tu yanayoulizwa (Magenau, 2004:39) na hivyo kumshauri wakili arekebishe swali au aulize swali tofauti. Matokeo ya kumwamuru mshitakiwa ajibu swali lile ni kwamba kauli yake ya 'hapana' ilitekeleza majukumu mawili: kwanza, kuthibitisha kauli ya uongo ya wakili kwamba alimwagiwa mchanga. Pili, kutoa jibu kwamba *hakuwa amelewa* wakati anamwagiwa mchanga. Madhara ya jibu alilotoa mshitakiwa yaweza kuwa kwamba aliongeza kiwango cha ukosaji wake machoni pa watoa maamuzi. Kufanya shambulizi ukiwa umelewa ni 'nafuu' kuliko kufanya kitendo hicho hicho ukiwa hujalewa. Kwa kutoa jibu hilo alionekana kustahili adhabu kali zaidi kwa kuwa alitenda kosa akiwa na akili timamu. Angekuwa ametenda akiwa amelewa, yaweza kuchukuliwa kwamba alikuwa ameghafirika kwa athari za ulevi tu, kwa hiyo kiwango cha ukosaji wake kinaweza kutazamwa kwa jicho la huruma kidogo. Na kwa kuwa mshtakiwa alikuwa anatuhumiwa kwa mauaji, alionekana kuwa mwenye roho mbaya sana kumshambulia mtu aliyekuwa amelewa na kumwua kwa kuwa tu eti yule mlevi alimwagia mchanga.

Kutokana na jinsi maswali yanavyoulizwa, ni vigumu wakati mwingine kuwa na hakika endapo muda wote mawakili hulenga anayehojiwa aelewe bila shaka yoyote kinachoulizwa ili lipatikane jibu sahihi. Tatizo la uelewa wa swali huwapo hata mahojiano yafanywapo kwa Kiswahili. Katika kesi hiyo hiyo ya Jinai namba 95 ya 2008, shahidi mmoja pia alikosa msaada wa jaji, labda kutokana na mtazamo wa wengi, wakiwamo watunga sera – kwamba Kiswahili ni lugha ya kila Mtanzania. Hebu tutazame kipande kifuatacho, ambacho ni sehemu ya mahojiano kati ya wakili na shahidi:

> **WAKILI:** Nani aliamua?
> **SHAHIDI:** (kimya akimtazama wakili)…Gesase
> **WAKILI:** Nakuuliza, nani aliamua?
> **SHAHIDI:** Chacha Makene
> **WAKILI:** Eti nani aliamua?
> **SHAHIDI:** (kimya, anaanza kufadhaika)…

Yawezekanaje kwamba shahidi anadai alikuwapo kwenye tukio halafu aulizwapo swali juu ya kitu dhahiri ababaike kwa kutoa majibu yanayopingana na hatimaye ageuke bubu? Kufuatia hali hii, jaji, mawakili na wazee wa baraza walichagua kupigwa butwaa. Ndiyo maana ulipofika wakati wa wazee wa baraza kuuliza maswali, mzee wa baraza #3 aliuliza swali ambalo linatia shaka juu ya uelewa wa baadhi ya washiriki katika maamuzi mahakamani. Alimuuliza shahidi: "Ushahidi wako unaonekana dhaifu, kweli si kweli?" Tukirudi kwa shahidi, swali chochezi ni: Je, kwaweza kuwa na tatizo lolote hapa kwa upande wa shahidi? Ushahidi alioutoa unaweza kuonekana dhaifu kutokana na kuufumbia macho ukweli niliotaja hapo juu, kwamba Kiswahili si lugha mama ya kila Mtanzania, na kwamba si kila azungumzaye Kiswahili ana ujuzi wa kutosha kukielewa na kukitumia katika mazingira tofauti tofauti. Hapa tunaweza kuazima mfano wa Jacquemet juu ya ushiriki wa ma-pentiti di camorra mahakamani. Jacquemet anasema kwamba mbali na kwamba ma-pentiti di camorra huongea Kiitaliano, walishindwa kuwasiliana kiufasaha mahakamani Italia kwa kuwa walitegemea Kiitaliano walichokuwa wanaongea mitaani. Anasema kwamba mapungufu ya lugha yanafanya wanaotoa maamuzi wawe na mtazamo hasi na shahidi (Jacquemet, 1992:113). Ni kweli, baada ya shauri mahakamani mmoja wa wazee wa mahakama aliniambia, "Shahidi huyu alikuwa amepandikizwa" ambayo huashiria kwamba kusingekuwa na juhudi yoyote kuzielewa changamoto zilizokuwa

zinamsibu. Swali aliloulizwa shahidi ni "Nani aliamua?" Je, ni kwa nini shahidi aliwataja Gesase na Chacha Makene badala ya mtu mwingine?

Tuanze kwa kumtazama shahidi. Kwanza, kwa jinsi shahidi alivyokuwa akijieleza kwa Kiswahili, ilikuwa dhahiri kwa mtu yeyote anayefuatilia masuala ya lugha kwa karibu kwamba uelewa na uwezo wake wa kutumia lugha ya Kiswahili ulikuwa mdogo sana, na alikuwa umeathiriwa kwa kiasi kikubwa na lugha yake ya asili ya Kikurya. Akiwa na umri chini ya miaka 40, kwa mfano, shahidi analitaja jina lake linaloanza na sauti /p/ (kama vile Paulo, Pio, Pendo) kwa kutumia sauti /b/ (kama vile Bhaulo, Bhio, na Bhendo), ambayo si kawaida kwa vijana wa Kikurya wanaokijua na kukiongea Kiswahili kwa ufasaha. Pili, na ambacho ni muhimu zaidi, katika maeneo atokayo shahidi neno lililozoeleka zaidi kwenye mazingira ya kujenga utulivu palipo na ugomvi ni 'kuachanisha' ugomvi, japo neno 'kuamua' nalo hutumiwa na wachache. Twaweza kusema kwa kiwango cha juu cha hakika kwamba lingetumika neno 'kuachanisha' badala ya 'kuamua', majibu ya shahidi yangekuwa tofauti na aliyotoa. Tuyatazame maswali yafuatayo (ambayo naamini mojawapo lilistahili kutumika baada tu ya shahidi kuanza kubabaika), na kisha tujaribu kuona wigo wa majibu ambayo yangetolewa:

1) "Nani aliyeachanisha ugomvi?"
2) "Nani alifanya ugomvi ukaisha?"
3) "Ugomvi uliishaje?"

Swali la kwanza hapo juu lingeweza kujibiwa kwa kutaja moja au zaidi ya majina ya watu, kama ilivyokuwa kwa swali lililoulizwa na wakili. Utofauti wa swali hili na alilouliza wakili ni kwamba kitenzi kilichotumika hapa kimezoeleka zaidi kwenye mazingira atokayo shahidi. Kwa hiyo lingeulizwa hili ingeweza kuwa rahisi kwa shahidi kutoa majibu ya hakika zaidi, bila kujali ukweli au uongo unaoweza kuwapo kwenye majibu yake. Kwa hatua ya mbele zaidi, endapo lingetumika swali namba 2) majibu yake yasingekuwa sawa na yale ya swali namba 1) pamoja na lile lililoulizwa na wakili. Hata hivyo, hapa asingekomea tu kuwataja washiriki pekee wa ugomvi kama waliofanya ugomvi ukaisha. Shahidi angeweza hata kumtaja mtu aliyeingilia kati kuumaliza ugomvi. Hali kadhalika, swali namba 3) lisingeleta utata wowote endapo shahidi alishuhudia tukio. Utofauti wa swali hili (la 3) na mengine yote ni kwamba halimdai shahidi ataje mtu. Yawezekana pia kwamba mmoja wa wagomvi alikimbia kwa hiyo

ugomvi ukaisha, na hivyo si lazima awe ameshiriki mtu wa tatu kufanya ugomvi uishe. Maswali mengine mawili yanajenga hoja kwamba lazima kuna mtu wa tatu alishiriki kufanya ugomvi uishe.

Katika mazungumzo ya jumla kuhusu ugomvi, Gesase na Makene (anaowataja shahidi) ndio waliopigana kabla Mwita Sangali hajajishirikisha na ugomvi huo. Kwa mazingira kama haya, 'aliyeamua' yaweza kuwa imechukuliwa na shahidi, japo kimakosa, kumaanisha 'nani aliyeamua kupigana', *kuamua* hapa ikiwa sawa na neno la Kiingereza *decide.* Hii yawezekana kuwa sahihi kwa kuwa hatimaye wote wawili aliowataja katika majibu yake, Gesase na Makene *waliamua kupigana* bila ushawishi wa mtu mwingine. Gesase (aliyekuwa amefanya sherehe nyumbani kwake na kuwaalika ndugu na rafiki zake) *aliamua* kupigana na Makene kwa sababu alichukizwa na kitendo cha Makene 'kulazimisha' [ishara ya dharau] kuondoka na *maganda* (chupa za bia). Kwa upande wake, Makene yeye *aliamua kupigana* na Gesase (mwenyeji wake) kwa kuwa aliona Gesase anamshushia heshima kwa kumzuia kuondoka na chupa mbili tu za bia, kwa kudai kwamba asingeweza kurudisha chupa tupu. Makene alinukuliwa akisema kwamba maganda hayakuwa na thamani kubwa kiasi cha Gesase kukosa imani kwamba hayatarudishwa. Labda ilimchukiza zaidi Makene kwamba alikuwa haaminiki wakati kwenye sherehe hiyo alikuwa ametoa zawadi ya zaidi ya shilingi laki moja na nusu, ambayo ni kubwa kuliko kiwango kilichotolewa na washiriki wenzie. Chupa mbili za bia hazikuwa na thamani ya kutosha kufanya asiaminike. Kwa mazingira haya ni rahisi kuelewa kwa nini shahidi anawataja hawa wawili kama 'walioamua'.

Katika mazingira kama haya kwenye mahojiano, mstenokalikimu hapaswi kusoma tu haiba ya shahidi na hatimaye kuamua kwamba huyu hakuwa shahidi wa kuaminika. Ingekuwa sahihi zaidi kuamua juu ya ubora wa shahidi baada ya kuwa swali hilo limeulizwa kwa njia tofauti. Wakili aliyekuwa anamhoji shahidi asingeweza kumsaidia shahidi kwa kuwa yeye angependa zijitokeze nafasi nyingi zaidi ambazo shahidi anatoa majibu ya kujichanganya ili ushahidi wake uonekane dhaifu. Yawezekana kwamba jaji alishindwa kutoa msaada hapa kwa kuwa yeye mwenyewe hakuwa na kilichokuwa kinahitajika kwenye mazingira haya, au kama asemavyo Jacquemet (1992:113), alishakerwa na haiba na kiwango cha chini cha uwezo wa shahidi kuwasiliana mahakamani.

Kwenye Kesi ya Jinai namba 26 ya 2006, Jamhuri dhidi ya ACP Zombe na wengine 12, hakukuwa na matatizo kama yaliyowasibu mashahidi kwenye kesi ya Jinai namba 95 ya 2008, lakini napo pia kuliulizwa maswali ambayo nadhani yalistahili katazo la jaji. Kwa mfano, wakili akimhoji shahidi namba 18 ambaye ni mtaalam wa maswala ya picha na ramani katika Wizara ya Mambo ya Ndani, alimuuliza, "Shahidi, je, ni watu wangapi ofisini kwenu ambao ni wataalam wa masuala ya ramani ambao wewe hujui kwamba ni wataalam wa masuala ya ramani kama wewe?" Hata shahidi alipoomba swali lirudiwe, jaji hakugundua kwamba swali lilikuwa limemchanganya shahidi. Wakili mwingine pia alimhoji Shahidi 22 kama ifuatavyo:

> **WAKILI:** Shahidi, una vyeti kuthibitisha kwamba wewe ni mtaalam wa mambo haya?
> **SHAHIDI 22:** Ndiyo. Lakini sikuja navyo hapa.
> **WAKILI:** Hukuja navyo mahakamani? Kwani hukujua kwamba ulipaswa kuja navyo? Mahakama inawezaje kuamini kuwa wewe ni mtaalam? Unataka tukuamini kwa maneno matupu?

Pia, akimhoji Shahidi 15, wakili aliuliza

> Na je, huoni kama unaweza kuwa umefanya dhambi kuongopa? Kwa kuwa umekula kiapo na kwa sasa unaongea uongo. Maelezo yako ya sasa na uliyoongea polisi yametofautiana. Je, huoni unaiongopea mahakama?

Katika mifano hiyo hapo juu, maswali yaliyoulizwa yalilenga kuwatega wahojiwa. Katika mahojiano kati ya wakili na Shahidi 22 nalitazama zaidi swali la mwisho. Japo liliulizwa kwenye zamu moja kama swali moja, lilikuwa na vipengele vingi kama ifuatavyo:

1) Hukuja navyo [vyeti] mahakamani? (kuashiria hamaki/mshangao);
2) Hukujua kwamba ulipaswa kuja navyo? (swali 1);
3) Mahakama inawezaje kuamini kuwa wewe ni mtaalam? (swali 2);
4) Unataka tukuamini kwa maneno matupu? (swali 3).

Mbali na kwamba kipengele cha kwanza huashiria hamaki au mshangao wa wakili, nacho chaweza kujibiwa kama swali, na hivyo kufanya kuwe na maswali manne yaliyoulizwa kama swali moja. Wakati vipengele 1, 2, na 4 vinahitaji majibu mafupi ya *ndiyo/hapana*, kipengele cha 3 kinahitaji maelezo. Cha kujiuliza hapa ni: Je, katika hali hii shahidi ajibu kipengele kipi? Katika jibu lake, shahidi

alisema, "Hapana, nitavileta ukitaka." Neno 'hapana' linajibu kipengele kipi? Jaji alirekodi nini?

Swali aliloulizwa Shahidi 15 lina utofauti kidogo na aliloulizwa Shahidi 22 hapo juu. Swali hili linamtaka shahidi afanye tathmini ya kitendo chake na aseme endapo hadhani kwamba *ametenda dhambi.* Hii inafuatiwa na sababu zinazoonyesha udhambi wa shahidi ulikoanzia. Kutenda dhambi ni tofauti na kutenda kosa la kisheria. Neno *dhambi* huashiria kwamba shahidi kamkosea Mungu. Kwa kutumia neno hilo wakili anamtisha shahidi. Lakini pia katika swali hilo anamwonyesha shahidi kwamba mbali na kutenda dhambi, ametenda kosa kisheria, ameiongopea mahakama. Wakili anamtaka shahidi atoe tathmini juu ya kauli hii pia. Kwa hiyo swali hili lina sehemu mbili ambazo mshtakiwa anapaswa kuzikubali au kuzikanusha: 1) 'mshitakiwa ni mdhambi', na 2) 'anaiongopea mahakama'. Lakini kwa jinsi swali lilivyoundwa, linalazimisha jibu liwe, 'ndiyo' au 'hapana' bila maelezo yoyote. Kwa upande mwingine, hata hivyo, jibu alilotoa shahidi linaashiria tatizo jingine mbali na matumizi ya rasilimali lugha. Jibu lake linaanza na "Nimeshakueleza……" ambayo huashiria kwamba swali hili lilikwishajibiwa. Cha kujiuliza hapa ni: Je, swali moja linaruhusiwa kuulizwa mara ngapi na muulizaji huyo huyo kwa muulizwaji huyo huyo kabla ya jaji kuingilia kati?

Dhana ya *Symbolic Interaction* husisitiza kwamba maana ni muhimu sana katika kujenga tabia ya binadamu, na kwamba maana hizi hujengwa kutokana na mawasiliano baina ya watu. Wananadharia hawa husisitiza pia kwamba hakuna maana ya kitu zaidi ya ile kipewacho na binadamu. Jiulize: ungekuwa mahakamani kwenye nafasi ya mshtakiwa au shahidi ungeichukuliaje mahakama? Kwa nadharia hii, ambavyo ungeichukulia mahakama, hiyo ndiyo maana yako ya mahakama. Je, mahakama ingeonekana kwako kama chombo cha kutolea haki? Wewe ukiiona mahakama kwako kama chombo X, na mwingine akakiona kama X pia, hali kadhalika na wengineo wengi vivyo hivyo, kutakuwa na maana tofauti na ile ambayo imeandikwa kwenye vitabu na mamlaka iliyoanzisha mahakama. Kwa maana nyingine ni kwamba mahakama itajitambua tofauti, kama chombo cha haki wakati wengi waliokwishapita kwenye shughuli za kimahakama huichukulia kama chombo hasi, kandamizi. Kwa kuwa maana hizi husemwa kuwa za jamii, huweza kugandamizwa tu zisisikike, lakini haziwezi kufutwa kwa kauli, bali kubadili

mwenendo. Na kama wasemavyo wananadharia hawa, "maana hizi huathiri tabia" (LaRossa na Reitzes, 1993:136).

Dhamira ya pili ni *umuhimu wa kuijenga nafsi,* ambayo husema kwamba *binadamu hujijenga nafsi kupitia mawasiliano yao na wengine*. Tukiichukulia mahakama kupitia maafisa wake (jaji, hakimu, wakili) kama nafsi moja, tungeweza kusema kwamba yaweza kubadili tabia kutokana na jinsi inavyoonwa na wengine wanaowasiliana nayo. Lakini labda swali la msingi ni, je, kumekuwa na sauti ya kutosha kufanya mahakama ijue kwamba yenyewe ni chombo X? Ikijua, je, yenyewe yaweza kujirekebisha, au inahitajika nguvu ya nje? Labda stadi kama hii bado si yowe ya kutosha, lakini ni mwaliko kwa Idara ya Mahakama kuichukua jamii ya watanzania kama kioo chake, hatimaye iwe na alichokiita Charles Cooley, *looking-glass self*, kwani uwezo wetu wa kujiona unategemea na wengine wanavyotuona.

**Hitimisho**

Sera ya lugha ya mahakama inachangia kwa kiasi kupunguza ufanisi wa maafisa wa mahakama. Majaji wanapolazimika kusoma haiba ya shahidi huku wakifanya ustenokalikimu hujikuta wameshindwa kutekeleza jukumu la kuhakikisha kwamba mahojiano yanakwenda kiusahihi. Makala hii, hata hivyo imezua shaka juu ya kiwango cha uelewa wa lugha miongoni mwa wastenokalikimu, na kuashiria kwamba kiwango kisichoridhisha cha uelewa huu kinaweza kufanya haki za washiriki kupotea.

Kwa hiyo suala la lugha na sheria katika mazingira ya Tanzania laweza kugawanywa katika sehemu kuu mbili: Kwanza, ni ugumu wa utekelezaji wa sera ya lugha inayodai mwenendo wa shauri na maamuzi yaandikwe kwa Kiingereza hata mashauri yafanyikapo kwa Kiswahili. Sera hii inafanya utendaji unakuwa mgumu zaidi hasa pale ambapo hakuna vifaa vya kunasia sauti. Ustenokalikimu na madhara yake ni matokeo hasi ya sera ya lugha mahakamani. Makala hii imetilia shaka uwezo wa waamuzi kuitekeleza sera hii kwa ufanisi katika mazingira yaliyopo. Pili, ni uwezo wa watoa maamuzi kutambua ufedhuli uliojificha kwenye matumizi ya rasilimali lugha ambao unaweza kumfanya anayehojiwa asiweze kutoa utetezi kwa njia inayoridhisha. Hili linatiliwa mbolea na mtazamo potofu kwamba kila anayeongea Kiswahili anaweza kufanya mawasiliano kiufasaha kwa Kiswahili. Mwisho, na muhimu pia, ni kwamba hali hii yaweza

kuiathiri mahakama machoni pa wanajamii ambayo itaifanya ionekane kama mhimili usiojali.

**Marejeo**


Beach, W. (1985). Temporal Density in Courtroom Interaction: Constraints on the Recovery of Past Events in Legal Discourse. *Communication Monographs*, 52: 1–19.

Danet, B. (1980). Language in the Legal Process. *Law & Society Review*, 14: 445–564.

Dunstan, K. (1980). Context for Coercion: Analyzing Properties of Courtroom "Questions". *British Journal of Law and Society*, 7(1): 61–77.

Evidence Act, Cap 6R.E.2002. Dar es Salaam: Government Printers, 154–155.

Freedgood, L. (2002). Voicing the Evidence: The Pragmatic Power of Interpreters in Trial Testimony. Unpublished PhD Thesis, Boston University.

Gibbons, J. (2003). *Forensic Linguistics: An Introduction to Language in the Justice System.* Oxford: Blackwell Publishing Ltd.

Goodman, G. S., Tobey, A. E., Batterman-Faunce, J. M., Orcutt, H., Thomas, S., Shapiro, C. & Sachsenmaier, T. (1998). Face-to-face Confrontation: Effects of Closed-circuit Technology on Children's Eyewitness Testimony and Jurors' Decisions. *Law and Human Behavior*, 22(2): 165–203.

Hale, S. & Gibbons, J. (1999). Varying Realities Patterned Changes in the Interpreter's Representation of Courtroom and External Realities. *Applied Linguistics*, 20(2): 203–220.

Hirsch, D. (2001). The Trial of Andrei Sawoniuk: Holocaust Testimony under Cross-examination. *Social and Legal Studies*, 10(4): 529–545.

Jacquemet, M. (1992). "If he Speaks Italian it's Better": Metapragmatics in Court. *Pragmatics*, 2(2): 111–126.

Kirchheimer, O. (1969). *Political Justice – The Use of Legal Procedure for Political Ends*. Princeton, NJ: Princeton University Press.

Konradi, A. (1996). Preparing to Testify: Rape Survivors Negotiating the Criminal Justice Process. *Gender and Society*, 10(4): 404–432.

LaRossa, R. & Reitzes, D. C. (1993). Symbolic Interactionism and Family Studies. Katika P. G. Boss, W. J. Doherty, R. LaRossa, W. R. Schumm & S. K. Steinmetz (wah.). *Sourcebook of*

*Family Theories and Methods: A Contextual Approach*, 135–163.

Luchjenbroers, J. (1991). Discourse Dynamics in the Courtroom: Some Methodological Points of Description. *La Trobe University Working Papers in Linguistics*, (4): 85–109.

Magenau K. S. (2003). Jury Duty: Competing Legal Ideologies and the Interactional Negotiation of Authority in Jury Deliberation. Unpublished PhD Thesis, Georgetown University.

Magistrate Courts Act. (1984). Dar es Salaam: Government Printers.

Maley, Y. (1994). The Language of the Law. Katika J. Gibbons (mh.). *Language and the Law*. London: Longman.

Marshall, J., Marquis, K. H. & Oskamp, S. (1971). Effects of Kind of Question and Atmosphere of Interrogation on Accuracy and Completeness of Testimony. *Harvard Law Review*, 84(7): 1620–1643.

Matoesian, G. M. (1993). *Reproducing Rape: Domination through Talk in the Courtroom*. Chicago: Chicago University Press.

Penman, R. (1987). Discourse in Courts: Cooperation, Coercion and Coherence. *Discourse Processes*, 10: 201–218.

Rigney, A. C. (1999). Questioning in Interpreted Testimony. *Forensic Linguistics*, 6(1): 1350–1771.

Wahn, P. & Clayton, S. D. (1996). The Effects of Attorney Presentation Style, Attorney Gender and Juror Gender on Juror Decisions. *Law and Human Behavior*, 20(5): 533–554.

Walker, A. G. (1987). Linguistic Manipulation, Power and the Legal Setting. Katika L. Kedar (mh.). *Power through Discourse*. New Jersey: Ablex.

Wellman, F. L. (1999). *The Art of Cross-Examination*. Beijing: Hongqi Press.

Woodbury, H. (1984). The Strategic Use of Questions in Court. *Semiotica*, 48(3/4): 197–228.